

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO
MTIHANI WA UJIRANI KIDATO CHA PILI
KISWAHILI**

021

16/05/2023 MCHANA

MAELEKEZO

MUDA: SAA 2:30

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi (10)
2. Jibu maswali yote
3. Andika jina lako katika kila ukurasa wa karatasi yako ya kujibia

**SEHEMU A: UFAHAMU (Alama 15)
Jibu maswali yote katika sehemu hii**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa
 - i. Majibizano baina ya watu wawili au zaidi wanapozungumza ni ;-

A. Dayolojia	C. Hotuba
B. Mahubiri	D. Risala
 - ii. Katika sababu zifuatazo ni ipi si sahihi kuhusu matumizi ya kamusi?

A. Kujifunza lugha ya kigeni	C. Kujua maana ya maneno
B. Kusanifisha maneno mapya	D. Kujua tahajia za maneno
 - iii. Ipi ni seti sahihi ya vipera vya semi?

A. Methali, mizungu na maghani	C. Mafumbo, soga na maghani
B. Misemo, mafumbo na vigano	D. Nahau, vitendawili na mizungu
 - iv. Njia ipi ya uhifadhiwa fasihi simulizi inayoweza kupokea mabadiliko ya kwa haraka kati ya hizi?

A. Maandishi	. Vinasa sauti
B. Kichwa	. Kompyuta
 - v. Masumbuko ni kijana wa kiume na nimchapa kazi hodari katika kituo cha mabasi ya mikoani jijini Dododma mwenye umri wa miaka 29-34. Juzi mjomba wake alimshauri aoe lakini akasema bado yupo yupo kwanza. Kwa Kiswahili sanifu kijana ambaye hajaoa na umri wake una ruhusu kuoia huitwa.

A. Msela	C. Mgane
B. Mjane	D. Msimbe
 - vi. Mjomba wangu alipopewa taarifa za kumfuata mgonjwa alieugua gafla, alitoa sentensi iliochekesha watu wote waliomsikia kwa kuniambia nikaweke gari kwenye mafuta badala ya kusema ni kaweke mafuta kwenye gari. Kiisimu watu waliomcheka mjomba kwa kuwa alifanya kosa ni lipi?

A. Kosa la kimofolojia	C. Kosa la kisarufi
B. Kosa la kimatamshi	D. Kosa la kimantiki

- vii. Wanafunzi waliofunga shule mwaka jana, baadhi yao walipanda mabasi **ya mikoani** kuelekea nyumbani kwao. Chunguza vizuri neno lililokolezwa kama lilivyotumika katika tungo hii kisha ubainishe linapatikana kwenye aina gani ya kivumishi kati ya hizi.
- A. Kivumishi cha idadi
B. Kivumishi cha a-unganifu
C. Kivumishi cha pekee
D. Kivumishi cha jina kwa jina
- viii. Mwalimu Hassan aliwauliza wanafunzi wa kidato cha kwanza wakakosa jibu kuntu kwa swali lililosomeka; "Katika lugha ya mazungumzo ni kitu gani kisipozingatiwa hulifanya neno barabara liwe na uvulivuli?" wewe ukuwa kama gwiji wa Kiswahili wa kidato cha pili bainisha jibu sahihi hapo chini
- A. Shadda
B. Kiimbo
C. Kidatu
D. Lafudhi
- ix. Malizia methali ifuatayo, Biashara.....
- A. Haina upinzani
B. Akili
C. Ni ujanja
D. Haigombi
- x. Fungu la sauti zinazotokea katikati au mwishoni mwa mstari wa shairi huitwaje?
- A. Vina
B. Vituo
C. Mizani
D. Silabi

2. Chagua kifungu cha maneno kutoka orodha B ambacho kinatoa maelezo sahihi ya neno/maneno yaliyopo kwenye orodha A. kisha andika herufu ya jibu sahihi.

ORODHA A	ORODHA B
<p>I. Utani II. Majigambo III. Mandhari IV. Ngano, visasili, tarihi V. Michezo ya watoto</p>	<p>A. Hadithi fupi zinazosimulia asili ya watu, vitu n ahata wanyama B. Mtambaji wa kazi za fasihi simulizi C. Mafumbo yanayohitaji kufumbuliwa D. Vipera vya tanzu za hadithi E. Mbinu anazotumia msanii ili kufukisha ujumbe kwa hadhira F. Kujisifu kunakoambatana na matendo G. Vipera vya tanzu za semi H. Maneno ya mzaha pasipo kuchukia I. Aina ya Sanaa inayotumia lugha inapowasilishwa kwa hadhira J. Mazingira/mahali inapofanyika kazi ya fasihi K. Shughuli zinazofanywa na watoto kwa lengo la kujiburudisha L. Watazamaji wa kazi ya fasihi</p>

SEHEMU B (Alama 70)

Jibu maswali yote kutoka sehemu hii

3. Wakati mwingine mtumiaji wa lugha huifanya lugha ifanane na kinyonga abadilike rangi kuendana na maeneo yamzungukayo. Kwa kujikita katika muktadha huo bainisha mambo manne (4) ya msingi yanayopelekea mtumiaji wa lugha kuipa tabia za ukinyonga lugha yake atumiayo.
4. Mzee fasihi ni mwenyekiti wa mtaa wa kichangani aliyeoa wake wawili, mke wa kwanza ni simulizi na mke wa pili ni andishi. Mke wa kwanza wa mzee fasihi ana watoto wanne ambao wa kwanza ni hadithi, wa pili ni semi, wa tatu ni maigizo na wanne ni ushairi.fafanua vijukuu vitano vya mzee fasihi kutoka kwa mtoto wake wa kwanza.
5. Babu Kiswahili ni msomi wa zamani ambaye mara kwa mara huonekana akifanya harakati za kuwakanya vijana wenye hulka za kutumia Kiswahili kisichofaa. Ukiwa kama msomi wa lugha, fafanua manufaa matano (5) yanayopatikana endapo harakati za babu Kiswahili zitafanikiwa kwa asilimia mia moja.
6. Watoto wengi katika jamii zetu hupendelea kucheza michezo mbalimbali pasipo kujua faida ya michezo hiyo. Wewe kama gwiji na nguli wa Kiswahili eleza faida za michezo ya watoto. Toa hoja tano (5)
7. Vijana wengi wakati mwingine hutumia maneno yasiyosanifu yanayozuka na kutoweka katika kipindi fulani cha maisha wakidhani kuwa ni lugha sanifu.wewe ukiwa kama mbobezi wa lugha .Fanya mambo yafuatayo;
 - A. Tambulisha jina la kiisimu la maneno hayo.
 - B. Tathmini njia nne (4) ambazo hutumia kuundia maneno hayo
 - C. Tathmini sababu tatu (3) ambazo hua ni msukumo kwa vijana kutumia maneno hayo
 - D. Bainisha madhara au hasara mbili (2) zinazoweza kujitokeza kutokana na kutumia maneno hayo
8. Ukiwa mtaalamu wa Kiswahili uliebobea na unaeaminika darasani kwako. Bainisha kipera cha fasihi simulizi kinacholingana na maelezo yaliyopo chini.
 - i. Hadithi fupi zinazosimulia asili ya watu, wanyama na vitu visivyo na uhai
 - ii. Semi fupi zenye mafunzo zinazohitaji majibu
 - iii. Semi zinazozuka katika jamii kwa kutaka kueleza hali na matukio mbalimbali yanayotokea kwa wakati huo.
 - iv. Maneno ya mzaha na ucheshi yanayoongelewa kati ya mtu na mtu , kabila na kabila na ukoo na ukoo
 - v. Sala au ibada inayowasilishwa kwa mungu au miungu ikiambatanishwa na sadaka kwa ajili ya kuomba uponyaji, kukinga magonjwa, majanga ya njaa na ukame.

9. Mwanahamisi ni mwanafunzi wa kidato cha pili asieweza kabisa kubainisha matumizi ya rejesta kulingana na muktadha mbalimbali. Msaidie mwanahamisi kubainisha muktadha wa wa utokeaji wa rejesta zifuatazo:-

- I. Funga goli! Mwanga yuko mbele, tutapigwa bao. Muktadha wa
- II. Jamaa alichukua mvua tatu, du! Tutamsahau kabisa. Muktadha wa
- III. Mheshimiwa; kwa idhini yako naomba kuwasilisha ushahidi ufuatao mbele yako. Muktadha wa
- IV. "Nani wali ng;ombe nani wali.....mbuzi.....muktadha wa.....
- V. Haya wote tusimame ni wakati wa kusifu sasa. Muktadha wa

SEHEMU C (Alama 15)

10. Wewe ni mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule ya sekondari Mawenzi, S.L.P 250, morogoro. Uma matatizo ya kiafya, hivyo umahitaji kwenda kutibiwa hospitali ya mkoa wa morogoro. Andika barua kwa mkuu wako wa shule kuomba rufusa ya siku mbili (2). Barua yako ipitie kwa mwalimu wako wa darasa. Jina lako liwe Kipepeo Jungu.